A

# NARCO yamsimamisha meneja tuhuma za upotevu ng'ombe 32

**Na Mwandishi Wetu,**

KAIMU Mkurugenzi Mkuu wa Kampuni ya Ranchi ya Taifa (NARCO), Masele Mipawa, amemsimamisha kazi Meneja wa Ranchi ya West Kilimanjaro iliyopo Arusha, Hezron Kyaruzi, kwa tuhuma za kukosa uadilifu kwa mali za umma na kusababisha upotevu wa ng'ombe takriban 32.

Akiwa katika ziara ya kutembelea Ranchi hiyo mwishoni mwa wiki, Mipawa alisema kuwa waliamua kufanya uamuzi huo kufuatia changamoto nyingi zinazoikumba shamba hilo ambazo kwa kiasi kikubwa zimechangiwa na uongozi mbovu wa meneja huyo.

"Kutokana na upotevu wa ng'ombe, uzembe na ukosefu wa maadili tumeamua kumsimamisha kazi Meneja wa Ranchi na msaidizi wake na hatua nyingine za kisheria na kinidhamu zitafuata," alisema Mipawa.

**Ziara hii imetusaidia kubaini kuwa kuna wizi uliokithiri katika shamba hili ambao umechangiwa na uhusiano mbovu kati ya meneja na jamii inayozunguka shamba hili.**

Mipawa alisema ziara hiyo aliyoifanya katika Ranchi hiyo ni kufanya ukaguzi kutokana na taarifa walizokuwa wakizipata ambazo zilionesha kuwa katika shamba hilo kumetokea upotevu wa ng'ombe ambao NARCO haina taarifa nao.

"Ziara hii imetusaidia kubaini kuwa kuna wizi uliokithiri katika shamba hili ambao umechangiwa na mahusiano mabovu kati ya meneja na jamii inayozunguka shamba hili, ukosefu wa maadili na uadilifu wa Meneja ambao umepelekea ng'ombe 32 kupotea," alisema.

"Kati ya ng'ombe hao 32 walipotea 15 wameshapatikana na wengine 17 hawajapatikana mpaka sasa huku ng'ombe wengine 27 walichinjwa bila kibali cha makao makuu," alifafanua Mipawa.

Kufuatia hali hiyo, Mipawa alisema wameamua pia kumsimamisha kazi msaidizi wake kwa kuwa alishindwa kumshauri vizuri meneja huyo, huku ikidaiwa alikuwa akishirikiana na meneja huyo kwenda kuazima ng'ombe kwa watu binafsi ili ranchi hiyo ionekane ina idadi kubwa ya ng'ombe.

Aidha, Mipawa aliwataka wafanyakazi wengine waliobaki katika shamba hilo kuendelea kufanya kazi kwa bidii, wazingatie nidhamu na uzalendo huku akiwaonya kuwa Serikali ya haitavumilia mtu yeyote anayehujumu rasilimali za Taifa.

HABARI LEO UK 5.

# Taasisi zatakiwa kuboresha uzalishaji mifugo

**Na Magnus Mahenge**

TAASISI za uzalishaji mazao ya mifugo nchini zimetakiwa kuboresha mifugo yao iuzwe katika soko la kimataifa likiwepo soko la nyama ya mbuzi Dubai katika Falme za Kiarabu (UAE).

Akitoa majumuisho baada ya ziara Taasisi ya Utafiti wa Mifugo Tanzania (TALIRI), Katibu Mkuu Wizara ya Mifugo na Uvuvi, (Mifugo) Profesa Olesante ole Gabriel alisema wakati umefika kuboresha mifugo kushinda soko la nje ya nchi ambalo linataka mazao ya mifugo bora.

Alizitaja taasisi za mazao ya mifugo ni Taliri, Bodi ya Nyama na Bodi ya Maziwa, Ranchi ya Mifugo Tanzania (NARCO) na zinazohusika na mazao ya mifugo nyama, maziwa na ngozi, kuweka mikakati mahususi kuboresha mifugo kwa ajili ya kukamata soko la nje ya nchi.

Alisema, serikali kwa kujua umuhimu wa fursa hiyo, Oktoba mwaka huu itaanza kuangalia uwezekano wa kupeleka nyama ya mbuzi soko la Dubai linalohitaji nyama bora lakini tamu.

Profesa Gabriel alisema kwa mahitaji makubwa ya soko hilo, taasisi hizo zikiboresha mazao ya mifugo hasa nyama zitapata fursa kubwa katika soko hilo wakati huu mazao yataonekana yametoka Tanzania nchi ya uchumi wa kati.

"Kwa sasa Tanzania inashika nafasi ya tatu kwa utamu wa nyama, ikitanguliwa na nchi jirani, ingawa ukweli nyama tamu hiyo inayotoka nchi jirani na kuuzwa katika soko la Dubai, inatoka huku lakini huuzwa kupitia nchi jirani," alisema.

Alisema ubora wa mifugo unaanza na uzalishaji bora, hivyo Taliri ina wajibu wa kushirikiana na Narco kusambaza malisho bora kwa wafugaji ili kupata mazao bora ya nyama, maziwa na ngozi bora ambayo inauzika katika soko la kimataifa.

Profesa Gabriel alisema kuhakikisha Tanzania iliyoingia uchumi wa kati kabla ya 2025 inazidi kupanda hadi uchumi wa juu, kuna kila sababu taasisi hizo kuboresha na kuimarisha ubora wa mifugo ili kushinda katika soko hilo la nje.

Alisema kupandisha uchumi, lazima pia serikali, taasisi na wafugaji kuwajibika kwa kuachana na ufugaji wa zamani wa kufuga mifugo mingi iliyokonda na kuanza kufuga kiutafiti, kisasa na kisayansi michache inayolishwa nyasi bora.

Wasioneleka shule

goza genge la uhalifu katika muda tofauti kati ya Januari

si kweli.
Pia alidai kataka

kilichokuwa kimehifadhiwa katika benki hiyo.

HABARI LEO UK 8.

# Meneja asimamishwa kazi kwa upotevu ng'ombe 32

**Na Mwandishi Wetu**

KAIMU Mkurugenzi Mkuu wa Kampuni ya Ranchi ya Taifa (NARCO), Masele Mipawa (pichani) amemsimamisha kazi Meneja wa Ranchi ya West Kilimanjaro iliyopo Arusha, Hezron Kyaruzi kwa tuhuma za kukosa uadilifu kwa mali za umma na kusababisha upotevu wa ng'ombe takribani 32.

Akiwa katika ziara ya kutembelea ranchi hiyo mwishoni mwa wiki, Mipawa alisema waliamua kufanya maamuzi hayo kutokana na matatizo mengi yanayolikumba shamba hilo ambayo kwa kiasi kikubwa yamechangiwa na uongozi mbovu wa meneja huyo.

"Kutokana na upotevu wa ng'ombe, uzembe na ukosefu wa maadili tumeamua kumsimamisha kazi meneja wa ranchi na msaidizi wake



na hatua nyingine za kisheria na kinidhamu zitafuata," alisema.

Mipawa alisema ziara hiyo aliyoifanya katika ranchi hiyo ni kufanya ukaguzi kutokana na taarifa walizokuwa wakizipata ambazo zilionesha kuwa katika shamba hilo kumetokea upotevu wa ng'ombe ambao Kampuni ya Narco haina taarifa nao.

"Ziara hii imetusaidia kubaini kuwa kuna wizi uliokithiri katika shamba hili ambao umechangiwa na mahusiano mabovu kati ya meneja na jamii inayozunguka shamba hili, ukosefu wa maadili na uadilifu wa meneja ambao umesababisha ng'ombe 32 kupotea," alisema.

"Kati ya ng'ombe hao 32 waliopotea, 15 wameshapatikana na wengine 17 hawajapatikana mpaka sasa huku ng'ombe wengine 27 walichinjwa bila kibali cha makao makuu," alifafanua Mipawa.

Kutokana na hali hiyo, Mipawa alisema wameamua pia kumsimamisha kazi msaidizi wake kwa kuwa alishindwa kumshauri vizuri meneja huyo huku ikidaiwa alikuwa akishirikiana na meneja huyo kwenda kuazima ng'ombe kwa watu binafsi ili ranchi hiyo ionekane ina idadi kubwa ya ng'ombe.

Aidha, Mipawa aliwataka wafanyakazi wengine waliobaki katika shamba hilo kuendelea kufanya kazi kwa bidii, wazingatie nidhamu na uzalendo huku akiwaonya kuwa serikali haitavumilia mtu yeyote anayehujumu rasilimali za taifa.

Scanned with CamScanner

Eric Kidyalla, one of CCM's aspirants for Dar es Salaam's Kibamba parliamentary seat in the upcoming (late October) General Election, "sells" himself at a nomination meeting held in the constituency yesterday. Photo: Correspondent Miraji Msala

THE GUARDIAN . Page 3.

# NARCO suspends its manager in Arusha over loss of cattle

By Guardian Reporter

THE Managing Director of the National Ranching Company (NARCO), Masele Mipawa, has suspended the manager of West Kilimanjaro ranch, in Arusha Region, Hezron Kyaruzi, for lack of safeguard to state property and loss of 32 head of cattle.

During his visit at the West Kilimanjaro ranch at the weekend Mipawa said he came up with the decision following many challenges facing the ranch due to poor leadership by the manager, and added that more legal and disciplinary measures will follow.

Mipawa said his inspection visit at the ranch was spurred by reports that showed loss of cattle of which NARCO had no official knowledge.

"The visit has helped us know that there is rampant theft at the ranch due to poor relations between the manager and the surrounding community, lack of professionalism and diligence on his part that caused the loss of 32 head of cattle," he said.

He added: "Out of the 32 animals that were lost, 15 have been recovered while 27 others were slaughtered without permission from the Head office,"

Mipawa said they have also decided to suspend Kyaruzi's for failing to well advise him with claims that he was also collaborating with Kyaruzi by going to private people to loan their cattle to show the ranch has a big number of cattle.

Mipawa called on other workers at the ranch to continue working hard, with discipline and patriotism and cautioned them that the Phase V Government will not tolerate any one sabotaging public assets.

well as inmates
"Amendment
Procedure Act
20 has inser
the reconcilia
strengthen set
logs and cong
police stations,
system," he sai
He also tol
received the tr
by showing g
procedure wh
train their co
The train
Mwakapun
training is
members
Iringa r
with cri
"He sa

Embassy of Sweden

Scanned with CamScanner